## SHULE YA WILAYA YA FRANCIS HOWELL

# KANUNI ZA MAADILI MEMA YA WANAFUNZI

Francis Howell School District
HOME SCHOOL COMMUNITY
LEARNING TOGETHER



# FAHARASA

**Utangulizi** ........ 3

**Miongozo ya Nidhamu Darasani** ........ 4

**Utangulizi wa Makosa na Viwango vya Kitabia** ........ 5

**Makosa ya Kitabia** ........ 6-10

**Ufafanuzi wa Viwango** ........ 11

**Kanuni za Wanafunzi za Matumizi mabaya ya Pombe/Dawa za Kulevya** ........ 12-13

**Kanuni za Shule Bila Silaha** ........ 14

**Ufafanuzi wa Nidhamu** ........ 15-17

**Miongozi ya Nidhamu katika Basi** ........ 18

**Adhabu za Viboko: Vitu zilizopigwa Marufuku** ........ 19

**Miongozo ya Matumizi Yanayokubalika ya Mtandao na Intaneti** ........ 20

**Kamusi ya Maneno** ........ 21-22

# UTANGULIZI




**MAZINGIRA MEMA, YENYE HESHIMA YA SHULE NI MUHIMU KWA ELIMU**
Kila mtu anatamani shule yake iwe mahali pa kukaribisha, pazuri, na penye heshima. Kwa kufanya kazi pamoja, wanafunzi, wazazi/walezi, wafanyakazi, na jamii wanaweza kufanya shule yao kuwa mahali pazuri pa mafunzo. Mwalimu mkuu anawajibika kudumisha mazingira mazuri ya kusoma. Wanafunzi wanaweza kusaidia kwa kukumbuka:

- Kuwa salama, kuwajibika, na kutulia
- Kuwaheshimu wanarika na watu wote wazima
- Kuheshimu mali zote za shule
- Kuwa shuleni na darasani kwa wakati unaofaa
- Kuwa tayari kwa darasa, pamoja na kazi na vifaa
- Kushiriki katika masomo yao
- Kuwa wakarimu na watumie lugha inayofaa
- Kuvaa vizuri
- Kufuata kanuni za shule na za waalimu wao
- Kuheshimu na kukubali utofauti kati yetu
- Kuonyesha jinsi wanavyohisi au wanachohitaji kwa njia zinazosaidia na zinazofaa
- Kutatua kutoelewana kwa njia zinazokubalika

**MISAADA YA TABIA NZURI KATIKA SHULE NZIMA (SWPBIS)**
Shule tisa (9) zimeanza kutumia PBIS ya Shule nzima kama mbinu ya kufunza tabia zinazokubalika na kuwasaidia wanafunzi ambao wanahitaji msaada wa ziada. Shule zote zimeweza kutambuliwa katika ngazi za jimbo.

**ELIMU YA TABIA**
Shule nyingi za FHSD zina mipango iliyowekwa vizuri ya Elimu ya Tabia ambayo inafanyakazi ili kuunda “jamii inayojali ya wanafunzi” kwa sifa nzuri za kitabia katika vijana kupitia maendeleo ya kiakili, kijamii na kimaadili. Wilaya ina shule tatu (3) ambazo zilipokea uteuzi wa Missouri School of Character na shule mbili (2) ambazo ziliweza kutambuliwa kwa National School of Character

**KIONGOZI NDANI YANGU**
Shule kadhaa za FHSD zimeanza kutumia mpango wa Covey wa Kiongozi Ndani Yangu (Leader in Me) kama njia ya kukukaza uongozi katika wanafunzi. Kulingana na kitabu cha *The 7 Habits of Highly Effective People*, mpango wa Kiongozi Ndani Yangu huwaandaa wanafunzi na ujasiri wa kibinafsi na ujuzi wanaohitaji ili kufanikiwa katika uchumi wa karne ya 21. Shule za Kiongozi Ndani Yangu huripoti kwa mfululizo utamaduni ulioimarika wa shule na kwa kupungua kwa ujumla kwa matatizo ya kinidhamu.
Kanuni za Maadili Mema ya Wanafunzi wa Shule ya Francis Howell inaelezea tabia ya wanafunzi ambayo huzingatiwa kuwa haifaii au sumbufu. Inatoa pia taratibu mbalimbali ambazo zinaweza kutumiwa kuzuia tabia kama hiyo na hatua za kinidhamu ambazo zinaweza kuchukuliwa ikiwa wanafunzi wahusika katika tabia zilizotajwa. Wilaya ya Shule ya Francis Howell pia inaunga mkono matumizi ya taratibu za kuingilia kati ambazo zinawapa wanafunzi mwongozo, mwelekezo, na msaada wa kufanikiwa shuleni.

# MIONGOZO YA NIDHAMU DARASANI



Kuunda mahusiano mema na wanafunzi ndio msingi wa usimamizi fanifu wa darasa. Waalimu wana wajibu wa kudumisha mazingira ya darasa yanayofaa kwa elimu. Majadiliano ya kuimarisha jamii yanahimizwa na wilaya kama njia ya kuunda jamii inayojali ambayo inajitunza na kujifuatilia. Madarasa yenye mahusiano thabiti na mema kati ya wanafunzi na walimu hukuza mazingira husishi ya elimu. Tunaamini kwamba masomo hufanyika vizuri katika jamii ya elimu ambapo wanafunzi wanashirikiana kati yao na kukuza ujuzi wa kuwafanya kuwa tayari kwa jamii na kufanya kazi. Usumbufu darasani au mchanganyiko wa usumbufu ikiwemo, lakini haijakomea kwa, kuongea sana, kuwa mbali na kiti, kurusha vitu, kuwasumbua wengine, matumizi mabaya ya vifaa vya elektroniki, kupitisha vijikaratasi vya manukuu na/au vitendo vingine ambavyo vinatatiza mchakato wa elimu haukubaliwi. Kanuni za Maadili Mema ya Wanafunzi zitatumika pia kwa wanafunzi wanaosoma katika mazingira ya mtandaoni ya Wilaya. Makosa ya kitabia yatashughulikiwa kwa njia sawa kana kwamba mwanafunzi angekuwa akihudhuria shule.

**Hatua za Hatua ya Kinidhamu**

| | |
|---|---|
| Tatizo la Kwanza | Mwalimu anaongea na mwanafunzi |
| Tatizo Linaloendelea | Mwalimu anampa mwanafunzi onyo<br>Mwalimu anaweza kuwasiliana na wazazi/walezi |
| Tatizo halijatatuliwa baada ya onyo | Huenda mwalimu akachagua kumzuia au kuita<br>mkutano wa kutatua tatizo na mwanafunzi na/au wazazi/walezi |
| Tatizo halijatatuliwa baada ya kumzuia au mkutano. | Mwalimu anamwelekeza mwanafunzi kwa ofisi ya mwalimu mkuu |

**Sera ya Kuchelewa**

Uzuiliwaji utatolewa na mwalimu/mwalimu mkuu wakati wanafunzi wanafika darasani baada ya kengele kulia. Mara za kuchelewa ambazo zinasababisha uzuiliwaji zitabainishwa katika kiwango cha jengo. Baada ya kuchelewa mara kadhaa, wanafunzi wanaweza pia kuelekezwa ofisini kwa hatua zaidi za kinidhamu.

# UTANGULIZI WA MAKOSA NA VIWANGO VYA KITABIA



Sera za Wilaya ya Shule ya Francis Howell zimebuniwa ili kuchangia mazingira mema ya elimu yanayotumiwa kwa usalama, ufanisi na mafanikio ya kibinafsi. Kuwaweka wanafunzi na wafanyakazi salama wakati wa janga hili la COVID-19 kutakuwa mojawapo ya vipaumbele vya juu vya Wilaya mwaka huu wa masomo. Wanafunzi watatarajiwa kufuata itifaki zote za usalama (kutotangamana na watu, kuvaa barakoa, kupanda basi kwa njia inayofaa, n.k) zilizoangaziwa na Wilaya. Wafanyakazi watatoa makumbusho kuhusu kutotangamana na watu na matarajio ya kuvaa barakoa. Kuendelea kukataa kutii makumbusho na maombi kutasababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu na shule, hadi na ikiwemo mwanafunzi kuhitajika kujiandikisha kwa mpango wa mtandaoni wa Wilaya.

Kwa hivyo, chati kwenye kurasa zinazofuata zitaonyesha makosa ya kitabia kama yalivyofafanuliwa na Wilaya ya Shule ya Francis Howell na kiwango kinacholingana cha nidhamu.

Viwango vya matokeo vinaweweza kutofautiana kati ya shule ya msingi na ya sekondari. Ni muhimu kukumbuka kwamba lengo kuu la nidhamu ni kufunza tabia inayohitajika, inayofaa na kuzuia tabia isiyofaa baadaye.

Makosa ya kitabia yaliyoorodheshwa katika kurasa zinazofuata yatapitiwa na wanafunzi wote kwa njia ambayo inafaa umri. Wazazi wanahimizwa kupitia makosa hayo na watoto wao.

Safari za shule au shughuli nyingine za shule, zikiwemo zile za nje ya majengo ya shule, ziko chini ya utawala wa mfanyakazi aliyeteuliwa wa shule. Sera na masharti yote ya Wilaya yanatumika wakati wa shughuli hizi iwe ni wanafunzi wa shule ya msingi au ya sekondari wanaohusika (shule ya kati na ya upili). Wanafunzi watawajibika kulingana na Kanuni za Maadili Mema ya Wanafunzi kwa makosa yaliyofanyika wakati wa safari na shughuli za nje ambazo zilifanyika nje ya majengo ya FHSD.

FHSD inaweza na itachukua hatua za kinidhamu kwa matukio ambayo yalifanyika nje ya kampasi ikiwa kuna uhusiano na shule au ikiwa tukio hilo lilisababisha usumbufu kwa mazingira ya shule.

**KANUNI ZA MAADILI MEMA HAZIWEZI KUTARAJIWA KUORODHESHA AU KUELEZEA KILA MOJA YA KOSA AMBALO LINAWEZA KUHITAJI MATUMIZI YA HATUA ZA KINIDHAMU. HATA HIVYO, WILAYA INA HAKI YA KUTEKELEZA MATOKEO YOYOTE AMBAYO YANAWEZA KUFAA CHINI YA HALI HII, KULINGANA NA HALI, UKALI NA MARUDIO YA TABIA HUSIKA.**

# Makosa ya Kitabia

| Tabia Isiofaa au Sumbufu | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 |
|---|---|---|---|---|
| **TABIA ZOTE AMBAZO NI HATARI** | | | | |
| Kwa mpangilio mwema wa shule ambazo zinzoibuka na kuwa makosa. Huenda kategoria hii ikatumiwa kwa makosa ambayo hayako chini ya moja ya fafanuzi za makosa. | ● | ● | ● | ● |
| **TENDO LA UCHOMAJI WA MAKUSUDI** | | | | |
| Kuchoma kwa makusudi au bila kujali mali ya mtu mwingine. **Rufaa kwa watekeleza sheria itafanywa na usimamizi wa shule.** | | | ● Shule ya msingi | ● |
| **TABIA ZA KIKATILI** | | | | |
| Zinaweza kuchukuliwa kuwa makosa ya Kiwango cha 3 ikiwa zitachukuliwa kuwa mbaya sana na mwalimu mkuu/ mwakilishi. | | ● | ● | |
| **KUMSHAMBULIA MWANAFUNZI AU MFANYAKAZI MWINGINE** | | | | |
| Kupitia kutumia nguvu za kimwili na lengo la kudhuru kimwili. **Rufaa kwa watekeleza sheria itafanywa na usimamizi wa shule.** | | ● Shule ya msingi | ● | |
| **TISHIO LA BOMU** | | | | |
| Kutishia kulipua vilipuzi, ikiwemo vitishio vyovyote vilivyoandikwa au vya simu; kwa ufafanuzi wa Tishio la Kigaidi (ANGALIA KAMUSI YA MANENO). **Rufaa kwa watekeleza sheria itafanywa na usimamizi wa shule.** | | | | ● |
| **UDHALIMU** | | | | |
| Udhalimu ni hatua ya makusudi ya mtu au makundi ya watu ya kutoa vitisho, tabia ya fujo, au ya unyanyasaji ambayo inajirudia au inaweza kurudiwa na inayomfanya mwanafunzi kuwa na hofu ya usalama wake wa kimwili au wa mali; ambayo hutatiza utendakazi wa elimu, nafasi, au haki za mwanafunzi yeyote; au hutatiza shughuli za kawaida za shule. Udhalimu unaweza kujumuisha vitendo vya kimwili, vikiwemo ishara, au udhalimu wa maneno, kielektroniki, au mawasiliano ya kuandikwa, na tishio lolote la kulipiza kisasi kwa kuripoti vitendo vya udhalimu. Inaweza kuzingatiwa kama makosa ya Kiwango cha 2, 3 au 4 ikiwa yatachukuliwa mabaya sana na mwalimu mkuu/mwakilishi. | ● | ● | ● | ● |
| **UDANGANYIFU/WIZI WA MAANDISHI** | | | | |
| Ina adhabu ya sufuri kwenye mtihani/kazi na mwalimu humwarifu mzazi/mlezi na msimamizi kuhusu tatizo hilo; hujumuisha udanganyifu wa kielektroniki. Matukio kadhaa yanaweza kusababisha kosa la Kiwango cha 2. | ● | | | |
| **KUTOWAHESHIMU WANAFUNZI AU WATU WAZIMA** | | | | |
| Ikiwemo, lakini haijakomea kwa, maneno, namna ya sauti, ishara za uso, ishara au maonyesho yaliyoandikwa. | ● | | | |
| **TABIA YA KUTATIZA** | | | | |
| Tabia ambayo ina lengo la makusudi la kutatiza elimu au usafiri salama wa wanafunzi, ikiwemo, lakini haijakomea kwa, kuongea sana, kutokaa kwenye kiti, kurusha vitu, kuwasumbua wengine, kupitisha vijikarasi vya manukuu na/au vitendo vingine (k.m. michezo ya mizaha kwa mwanafunzi ) vinavyoathiri mchakato wa elimu. Mizaha kwa wanafunzi inaweza kuzingatiwa chini ya ukiukaji huu. Inaweza kuzingatiwa kama makosa ya Kiwango cha 2, 3 au 4 ikiwa yatachukuliwa mabaya sana na mwalimu mkuu/mwakilishi. | ● | ● | ● | |
| **USEMI AU TABIA YA KUDHALILISHA** | | | | |
| Ikiwemo, lakini haijakomea kwa, matumizi ya lugha ya chuki (iliyoandikwa au kunenwa) ili kuwadhalilisha watu wengine kwa sababu za umbari, rangi, jinsia, asili ya kitaifa, umri, jamii, ulemavu, dini, mapendeleo ya kingono au mwelekeo wa kingono unaoshukiwa (inaweza pia kusababisha rufaa ya Title IX au Title VI). Hii ni pamoja na tabia, usemi wa kunena, kuandika au wa ishara. Inaweza kuzingatiwa makosa ya Kiwango cha 3 ikiwa itachukuliwa kuwa ni mbaya sana na mwalimu mkuu/mwakilishi. | | ● | ● | |

# Makosa ya Kitabia

| Tabia Isiofaa au Sumbufu | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 |
|---|---|---|---|---|
| **UKIUKAJI WA SHERIA ZA MAVAZI** | | | | |
| Hali ya mavazi au mwonekano yanayokiuka sheria ya mavazi ya shule, zisizofaa kwa shughuli za shule na/au zinazotatiza mchakato wa ilimu, ikiwemo, lakini haijakomea kwa, kulegeza suruali/ nguo zinazofichua mwili, zinazofichua nguo za ndani, kuvaa viatu vya njumu na/au minyororo, au chapa zisizofaa kwenye mavazi/barakoa (k.m. Zinazodokeza ngono, dawa za kulevya, vinywaji vya kulevya, silaha, shughuli haramu, n.k.). Huenda waalimu wakuu wakauliza wanafunzi wawaambie wazazi walete mavazi yanayofaa ya kubadilisha. Ikiwa baada ya mwanafunzi kuambiwa abadilishe kwa mavazi ambayo yanatimiza sheria ya mavazi kisha mwanafunzi huyo apatikane tena kuwa anakiuka tena sheria hiyo ya mavazi, hatua za ziada za kinidhamu zinaweza kuchukuliwa. | ● | | | |
| **UKIUKAJI WA SHERIA ZA KUENDESHA GARI/KUEGESHA GARI** | | | | |
| Kuegesha gari katika maeneo yasioruhusiwa, kuegesha gari bila kibali, au kushindwa kutii maagizo yaliyowekwa kwa madereva wanafunzi. Kuendesha gari kwa njia ya kutojali katika eneo la maegesho. Kushindwa kutii kunaweza kusababisha kupoteza haki za kuegesha gari au matokeo mengine ya kinidhamu. | ● | | | |
| **MATUMIZI MABAYA YA VIFAA VYA KIELEKTRONIKI** | | | | |
| Matumizi au kuonyesha simu au vifaa vingine vya elektroniki visivyo vya elimu wakati wa saa zisizoidhinishwa za shule vikiwemo, lakini havijakomea kwa, vifaa vya masikio, iPods, DVD, visomaji pepe, nk. Wilaya haitawajibika kwa uharibifu, hasara au wizi wa vifaa hivyo. Hii inajumuisha matumizi yasiyofaa, yasioidhinishwa, kunasa, kupitisha au kurudufu picha isioidhinishwa ya wafanyakazi na wanafunzi wa shule, au hati za shule. Inapaswa kukumbukwa kwamba kupiga picha chooni au katika vyumba vya kubadilishia hakuruhusiwi na itachukuliwa kuwa makosa ya Kiwango cha 2 au 3. Vifaa vilivyochukuliwa vinaweza kuchunguzwa kwa ujumbe na/au picha zisizofaa. **Wanafunzi watawajibika kwa maudhui yaliyo kwenye simu haijalishi maudhui hayo yasiofaa yalitoka wapi.** Katika hali nyingine, matumizi ya vitu hivi yataruhusiwa na mwalimu kwa madhumuni ya elimu au kama vishawishi na msimamizi. | ● | | | |
| **MASHTAKA YA UWONGO** | | | | |
| Yaliyofanywa kwa makusudi dhidi ya wanafunzi au wafanyakazi. Yanaweza kuchukuliwa kuwa makosa ya kiwango cha 3 ikiwa yatachukuliwa kuwa ni mabaya sana na msimamizi wa jengo. | | ● | ● | |
| **MAONYO BANDIA/MATUMIZI MABAYA YA VIFAA VYA KUZIMA MOTO** | | | | |
| Kuchezea vifaa vya dharura au kuwasha king'ora cha maonyo bandia au kuwasilisha ripoti ya uwongo (k.m. kupiga simu kwa 911). Yanaweza kuchukuliwa kuwa Kiwango cha 3 ikiwa itachukuliwa kuwa ni mbaya sana na mwalimu mkuu/mwakilishi. | | ● | ● | |
| **KUPIGANA** | | | | |
| Kupigana wenyewe kwa wenyewe (tofauti na shambulizi) au kutumia maneno au vitendo vinavyochochea au kusababisha vita. **Kurekodi video na kushiriki kwa njia yoyote au kuchapisha video ya vita kwenye mitandao ya kijamii kunajumuishwa katika makosa haya.** Inaweza kuzingatiwa kuwa makosa ya Kiwango cha 3 ikiwa itachukuliwa kuwa ni mbaya sana na mwalimu mkuu/mwakilishi. | | ● | ● | |
| **FATAKI** | | | | |
| Umiliki au matumizi ya fataki. | | ● Shule ya msingi | ● | |
| **UGHUSHI** | | | | |
| Wa saini ya mzazi/mlezi (ikiwemo kumwiga mzazi kupitia kwa simu) mwalimu au saini rasmi (za ruhusa, za kuchukuliwa) n.k. | ● | | | |

# Makosa ya Kitabia

| Tabia Isiofaa au Sumbufu | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 |
|---|---|---|---|---|
| **MAGENGE/ISHARA ZA MAGENGE** | | | | |
| Mashirika ya siri au uanachama wa "klabu" ambao ni hatari kwa mpangilio mwema wa shule; Kuonyesha na/au kuandika alama au ishara za magenge. | | ● | | |
| **MAONYESHO YASIOFAA YA MAHUSIANO** | | | | |
| Maonyesho yasiofaa yanajumuisha kubusiana, kupapasana, n.k. | ● | | | |
| **KUONYESHA UCHI/KUVUA MAVAZI** | | | | |
| Hujumuisha kuonyesha makalio na/au sehemu nyeti katika maeneo ya umma au kumvua mtu mwingine au kujivua mwenyewe na kufichua sehemu yoyote ya siri ya mwili na/au nguo za ndani. Kuvuta chini suruali ya mtu mwingine "*Pantsing*" iko chini ya makosa haya. Inaweza kusababisha kuripotiwa kwa afisa wa masuala ya utifuu shuleni. Huenda ikazingatiwa kuwa Makosa ya Kiwango cha 3 kama itachukuliwa kuwa mbaya sana na mwalimu mkuu/mwakilishi. | | ● | ● | |
| **MIONGOZI YA KUONDOSHWA KWA MUDA SHULENI** | | | | |
| Kushindwa kutii miongozi ya Kuondoshwa Kwa Muda Darasani. | | ● | | |
| **KUTOTII (KUKAIDI MAMLAKA/HATUA YA MOJA KWA MOJA YA KUTOTII)** | | | | |
| Kukataa kufuata maagizo au maombi ya wafanyakazi, au kukaidi mamlaka ya wafanyakazi. | ● | | | |
| **UKIUKAJI KATIKA VYUMBA VYA KUBADILISHIA/VYOO** | | | | |
| Matumizi mabaya ya nyenzo za chooni (sabuni, maji, taulo za karatasi, karatasi za choo). Kuingia kwenye chumba cha kubadilishia au choo cha "jinsia tofauti" (ikiwemo kumsukuma mtu yule mwingine kwenye chumba cha kubadilishia au choo cha "jinsia tofauti") ni kosa la Kiwango cha 2. | ● | ● | | |
| **KUDANGANYANA** | | | | |
| Kutoa maelezo ya uwongo au yasio sahihi kwa kujua. | ● | | | |
| **KUTEMBEA ISIVYOFAA KATIKA MAJENGO** | | | | |
| Kushindwa kutembea kimya kwenye majengo; kutotembea kulingana na foleni; kukimbia katika jengo; kushindwa kutumia njia za moja kwa moja; kuondoka kwenye eneo ulilowekwa bila kibali. | ● Shule ya msingi | | | |
| **TABIA YA UZEMBE** | | | | |
| Kusababisha uharibifu kwa mali ya mtu mwingine au majeraha au kuhatarisha usalama wa mtu mwingine (ikiwemo, lakini haijakomea kwa, kushindwa kuvaa barakoa kama inavyohitajika ili kuzuia kuenea kwa COVID-19, matumizi ya vifaa vya kuchezea vya "mshtuko", ukiukaji wa usalama wa maabara, na tabia nyingine za kutojali). Mizaha ya wanafunzi inaweza pia kujumuishwa katika kategoria hii. | | ● | | |
| **DAWA UNAZONUNUA KWENYE KAUNTA** | | | | |
| **Umiliki** au matumizi ya, ikiwemo, lakini haijakomea kwa, dawa zinazoagizwa na daktari ni **makosa ya Kiwango cha 2.** Usambazaji, uuzaji au ununuzi wa (ikiwemo, lakini haijakomea kwa, dawa zinazoagizwa na daktari) au kuwa chini ya ushawishi wa dawa "zinazouzwa kwenye kaunti" zinazosababisha tabia sumbufu kwa mazingira ya elimu ni **makosa ya Kiwango cha 3.** | | ● | ● | |
| **MGUSANO WA KIMWILI/MADHARA YA KIMWILI** | | | | |
| gusano au tabia isiyofaa (k.m. kuburushana, mchezo wa kupigana, au kuchezeana kwa fujo). Madhara ya kimwili ni tabia kama vile "mchezo" wa kupigana, kugongana, kusukumana, kupigana makofi, ngumi, au mizaha ambayo ina uwezo wa kusababisha madhara ya kimwili kwa mwanafunzi au mtu mzima. Inaweza kuzingatiwa ukiukaji wa Kiwango cha 2 ikiwa itachukuliwa kuwa ni mbaya sana na mwalimu mkuu/mwakilishi. | ● | ● | | |

# Makosa ya Kitabia

| Tabia Isiofaa au Sumbufu | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 |
|---|---|---|---|---|
| **PONOGRAFIA** | | | | |
| Umiliki wa nyenzo ambazo zinachukuliwa kuwa ponografia au za uchi na/au za ngono ya waziwazi, ikiwemo picha/mawasiliano yaliyoandikwa au kifaa chochote cha elektroniki. **Wanafunzi wanawajibika kwa maudhui yote kwenye simu zao haijalishi maudhui hayo yalitoka wako.** Inaweza kuzingatiwa kosa la Kiwango cha 3 kwa kutegemea hali ya maudhui. | | ● | ● | |
| **UMILIKI, MATUMIZI AU KUWA CHINI YA USHAWISHI** | | | | |
| Wa pombe, vinywaji vya kimea "visivyokuwa na pombe" , dawa za kulevya, kemikali halali zisizoagizwa na daktari ambazo zinasababisha kudhoofika, dawa za kuagizwa na daktari, au dawa zilizothibitiwa; au dawa zinazowasilishwa kama pombe, vinywaji vya kimea "visivyokuwa na pombe", dawa za kulevya, kemikali halali zisizoagizwa na daktari ambazo zinasababisha kudhoofika, dawa zinazoagizwa na daktari au dawa zinazothibitiwa, au umiliki wa vifaa vya dawa (k.m. mizani, paipu) au vitu vinavyoonekana kuwa vifaa vya dawa vya kutumiwa kwa dawa za kulevya au zinazodhibitiwa (angalia KANUNI ZA WANAFUNZI ZA MATUMIZI MABAYA POMBE/DAWA ZA KULEVYA). **Rufaa kwa watekeleza sheria itafanywa na usimamizi wa shule.** | | | ● | |
| **UMILIKI WA MALI ILIYOIBIWA** | | | | |
| Umiliki wa mali iliyoibiwa yenye thamani ya $100.00 ni kosa la Kiwango cha 1 na $100.00 na zaidi ni kosa la Kiwango cha 2. | ● | ● | | |
| **UMILIKI WA REKODI/HATI/FAILI ZA WILAYA** | | | | |
| Wizi na/au ubadilishaji wa hati za Shule, rekodi za mwanafunzi, stakabadhi (ikiwemo, lakini haijakomea kwa, kuingia bila ruhusa kwa njia ya elektroniki na kupakua vitabu vya gredi, kadi za ripoti, programu au maunzi ya kompyuta, mitandao ya usimamizi, rekodi za kompyuta, manenosiri, nk.). | | | ● | |
| **SHUGHULI ZA KULETA FUJO** | | | | |
| Zaidi ya wanafunzi 2 wanaoshiriki katika vita au kitendo kingine chochote ambacho kinawakilisha kupigana au kusababisha vita. | | | ● | |
| **UKIUKAJI WA SHERIA** | | | | |
| Kushindwa kufuata sheria za kafeteria, uwanja wa michezo, chumba cha chakula cha mchana, ukumbi, kutotangamana na watu na hafla za shule. | ● | | | |
| **UUZAJI, KUSHIRIKI AU USAMBAZAJI** | | | | |
| Wa pombe, vinywaji vya kimea "visivyokuwa na pombe", dawa za kulevya, kemikali halali zisizoagizwa na daktari ambazo zinasababisha kudhoofika, dawa za kuagizwa na daktari, dawa zilizothibitiwa, dawa zinazoagizwa na daktari, au dawa zilizowasilishwa na muuzaji kuwa yoyote kati ya zilizotajwa hapa (angalia KANUNI ZA WANAFUNZI ZA MATUMIZI MABAYA POMBE/DAWA ZA KULEVYA). **Rufaa kwa watekeleza sheria itafanywa na usimamizi wa shule.** | | ● Shule ya msingi | ● | |
| **MWENENDO USIOFAA WA KINGONO** | | | | |
| Kujigusa mwenyewe au mwili wa mtu mwingine kwa nguvu, kwa makusudi, au kwa hiari na/au kuvaa nguo kwa njia mbayo inadokeza au inayosababisha mgusano wa kingono; hii inajumuisha ujumbe pepe wa "sexting". | | ● | | |
| **UNYANYASAJI WA KIMAPENZI NA/AU UNYANYASAJI AU UBAGUZI** | | | | |
| Kwa misingi ya umbari, rangi, jinsia, asili ya kitaifa, jamii, ulemavu, dini, mwelekeo wa kingono, au mwelekeo unaoshukiwa wa kingono au tabia yoyote nyingine iliyolindwa na sheria za jimbo na za serikali. Unyanyasaji wa kingono hufafanuliwa kama kusumbuliwa kingono, maombi ya fadhila za kingono, au mgusano wowote wa kimwili au maneno ya hali ya kingono. Hii inajumuisha maoni ya kusema, kuitana majina ya kingono, ishara, vichekesho, matusi, picha au barua zenye maudhui ya kingono, na kueneza uvumi wa hali ya kingono Unyanyasaji wa kingono utasababisha rufaa ya Title X kwa afisa wa utiifu wa jengo.  Inaweza kuzingatiwa ukiukaji wa Kiwango cha 3 ikiwa itachukuliwa kuwa ni mbaya sana na mwalimu mkuu/mwakilishi. | ● Shule ya msingi | ● | ● | |

# Makosa ya Kitabia

| Tabia Isiofaa au Sumbufu | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI MABAYA YA TEKNOLOJIA/MTANDAO** | | | | |
| Matumizi yasiofaa ya teknolojia/mtandao wa Wilaya. Ukiukaji wa "Miongozi Inayokubalika ya Matumizi“ ya Wilaya. Wanafunzi waliopewa teknolojia ya Wilaya ili kuwasaidia na kusoma katika mazingira ya mtandaoni wanaweza kuadhibiwa kwa kutumia vibaya teknolojia ya Wilaya. Wanaweza kuzingatiwa kwa makosa ya Kiwango cha 3 au 4 ikiwa itachukuliwa kuwa ni mbaya sana na mwalimu mkuu/mwakilishi. | ● | ● | ● | ● |
| **WIZI WA PESA AU MALI (YA UMMA AU YA KIBINAFSI)** | | | | |
| Wizi wa pesa au mali ya chini ya $100.00 ni makosa ya Kiwango cha 1. Wizi wa pesa au mali ya $100.00 au zaidi ni makosa ya Kiwango cha 2. **Wizi unaweza kusababisha rufaa kwa watekeleza sheria.** | ● | ● | | |
| **TISHIO LILILOTOLEWA KWA WATU 10 AU ZAIDI.** | | | | |
| Kwa ufafanuzi Tishio la Ugaidi (ANGALIA KAMUSI YA MANENO). **Rufaa kwa watekeleza sheria itafanywa na usimamizi wa shule.** | | | ● Shule ya msingi | ● |
| **KUTISHIA/KUTISHIA KUCHUKUA MAISHA YA MTU MWINGINE** | | | | |
| Kutishia mtu mzima au mwanafunzi kwa maneno au kimwili. Kiwango cha hatua ya nidhamu kitabainishwa kulingana na muktadha. Maoni ya kihisia hayatashughulikiwa kwa njia moja kama tishio lililopangwa na kuandikwa. Linaweza kuchukuliwa kama kosa la Kiwango cha 4 ikiwa itachukuliwa kuwa ni mbaya sana na mwalimu mkuu/mwakilishi. Usimamizi wa shule unaweza kuripoti kwa polisi. | | ● Shule ya msingi | ● | ● |
| **BIDHAA ZA TUMBAKU/UVUTAJI WA SIGARA/SIGARA YA ELEKTRONIKI** | | | | |
| Kumiliki, kuvuta au kutumia bidhaa yoyote ya tumbaku ikiwemo vifaa vya kuvuta sigara vya elektroniki, sigara za elektroniki, mafuta, viko, vibiriti, karatasi, vishawa sigara, n.k. kwenye mali yoyote ya shule kabla, wakati au baada ya saa za shule. Bidhaa za tumbaku zitatupwa mara moja, ikiwa ni pamoja na sigara za elektroniki. **Watekeleza sheria wanaweza kuandika ripoti kwa watoto wadogo wanaomiliki vifaa kama hivyo.** | | ● | | |
| **KUINGIA BILA RUHUSA SHULENI NA/AU KWENYE MAJENGO YA WILAYA** | | | | |
| Kuwa katika maeneo ya shule ukiwa umefukuzwa au wakati shule au shughuli haziendelei. | | | ● | |
| **UTORO** | | | | |
| Kutokuwepo darasani, wakati wa chakula cha mchana, wakati wa msaada wa lazima wa kielimu au siku ya shule bila kibali; ikijumuisha kuondoka maeneo ya shule bila kibali au kutopeana nukuu kutoka kwa mzazi au simu ya mzazi inayothibitisha kutokuwepo. | ● | | | |
| **UHARIBIFU** | | | | |
| Kidogo, unaohitaji muda wa ziada wa uangalizi wa kusafisha, fidia inaweza kujumuishwa; uharibifu wa makusudi au jaribio la kuharibu mali ya wafanyakazi, wanafunzi, au Wilaya (fidia itahitajika). Mizaha ya wanafunzi inaweza kuwa chini ya makosa haya. Inaweza kuchukuliwa kuwa ukiukaji wa Kiwango cha 3 ikiwa itachukuliwa kuwa mbaya sana na msimamizi wa jengo. | ● | ● | | |
| **KITENDO CHA UJEURI** | | | | |
| Cha mwanafunzi au mfanyakazi, anayejaribu ***kuuwa au kusababisha majeraha makali ya kimwili***—mwanafunzi kutumia nguvu za kimwili na lengo la kusababisha majeraha mabaya ya kimwili. **Rufaa kwa watekeleza sheria itafanywa na usimamizi wa shule.** | | | ● Shule ya msingi | ● |
| **UMILIKI WA SILAHA/BUNDUKI** | | | | |
| Umiliki wa au matumizi ya silaha (Ufafanuzi wa SILAHA katika KAMUSI YA MANENO) **Rufaa kwa watekeleza sheria itafanywa na usimamizi wa shule.** 12 | | | | ● |

# Ufafanuzi wa Viwango

| | | |
|---|---|---|
| **KIWANGO CHA 1** | **MIFANO YA MSAADA WA DARASANI NA HATUA YA USIMAMIZI** | |
| | Mkutano wa waalimu na mwanafunzi na kufundisha tena tabia inayofaa na/au kanuni za darasani | Kunyimana mapumziko - nusu/yote (inapaswa kutumiwa tu wakati ambapo hakuna njia nyingine za kuchukua hatua dhidi ya tabia ya ukiukaji) |
| | Nafasi za mafunzo-mazoezi mema | Msaada wa chakula cha mchana (Chakula cha mchana hakipaswi kunyimwa kamwe) |
| | Mawasiliano ya kunena/kuandika na wazazi/walezi yanayohusiana na tabia | Mkutano wa mwalimu/mzazi/mlezi na/au mwalimu mkuu |
| | Ripoti za kila siku/kila wiki zinazotumwa kwa wazazi/walezi kuhusu maendeleo | Utekelezaji wa misaada mbadala, kama vile chati ya kila siku, hatua za kurekebisha nidhamu |
| | Kufanya mabadiliko ya mtaala kama inawezekana | Kukataza haki maalum |
| | Kumchelewesha mwanafunzi baada ya shule | Uzuiliwaji wa Chakula cha Mchana/Mapumziko |
| | Kosa la KWANZA - Kuondoshwa kwa muda shuleni au kufukuzwa shuleni kwa hadi siku 3 | |
| | Kosa la PILI - Kuondoshwa kwa muda shuleni kwa hadi siku 5 | |
| | Kosa la TATU NA KUENDELEA - Kuondoshwa kwa muda shuleni kwa hadi siku 10 | |
| **KIWANGO CHA 2** | **MIFANO YA MSAADA KABAMBE NA HATUA YA USIMAMIZI** | |
| | Mkutano unaomhusisha mwanafunzi na mzazi/mlezi | Uzuiliwaji wa ndani ya shule - kupoteza haki za mapumziko/chakula cha mchana |
| | Mkutano wa mzazi/mlezi/mwalimu/mwanafunzi/msimamizi | Fidia na/au mkutano/nafasi za hatua za marejesho |
| | Uzuiliwaji Baada ya Shule | Rufaa kwa Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo na uwezekano wa siku za ziada za Kuondoshwa Kwa Muda Shuleni hadi siku 180 |
| | Kuondoshwa Kwa muda darasani au shuleni kwa hadi siku kumi (10) | Kufukuzwa kabisa |
| | Kosa la KWANZA - Kuondoshwa kwa muda shuleni kwa hadi siku 10 | |
| | Kosa la PILI - Kuondoshwa kwa muda shuleni kwa hadi siku 180 | |
| **KIWANGO CHA 3** | **KUONDOSHWA KWA MUDA NA RUFAA** | |
| | Kuondoshwa kwa Muda Darasani | |
| | Kuondoshwa kwa Muda Shuleni kwa hadi siku 180 | |
| | Kuwekwa katika Mpango Mbadala wa Kuingilia Kati katika shule tofauti | |
| | Rufaa kwa Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo na uwezekano wa siku za ziada za Kuondoshwa Kwa Muda Shuleni hadi siku 180 | |
| | Kufukuzwa kabisa | |
| | Makosa YOYOTE Yafuatayo ya Kiwango cha 3- Yanaweza kusababisha kufukuzwa kabisa | |
| **KIWANGO CHA 4** | **KUONDOOSHWA KWA MUDA NA RUFAA ZILIZOONGEZWA** | |
| | Kuondoshwa kwa Muda Darasani | Kuripotiwa kwa Kamati Inayohusiana na Mienendo ili kusikiliza kesi na uwezekano kuongezwa kwa siku za ziada za Kuondoshwa kwa Muda Shuleni hadi siku 180 |
| | Kuondoshwa kwa Muda Shuleni | |
| | Kufukuzwa kabisa | |
| | Ukiukaji wa Silaha—Kuondoshwa kwa muda kusiopungua mwaka mmoja (siku 365 za kalenda) au kufukuzwa kabisa, ubainishaji ukifanywa kulingana na Mo. Rev. § 160.261 | |

# KANUNI ZA WANAFUNZI ZA MATUMIZI YA POMBE NA DAWA ZA KULEVYA



Bodi ya Elimu inatambua mgao wake wa majukumu ya afya, maslahi na usalama wa wanafunzi wanaohudhuria Wilaya ya Shule ya Francis Howell. Kwa hivyo, matumizi, mauzo, uhamishaji, umiliki au kuwa chini ya ushawishi wa pombe au dawa za kulevya umepigwa marufuku kwenye majengo ya shule, katika shughuli au matukio yanayodhaminiwa na shule, kwenye safari za nje, au ndani ya gari lolote linalotumika kuwasafirisha shuleni wanafunzi wa wilaya.

**Pombe**, kama inavyoyumiwa katika Kanuni hii ya Maadili Mema ya Wanafunzi, inaelezewa kama vinywaji vya pombe, vinywaji vya kimea “visivyokuwa na pombe” au dawa zozote zilizowasilishwa kuwa pombe au vinywaji vya kimea “visivyokuwa na pombe”.

**Dawa za kulevya**, kama ilivyofafanuliwa katika Kanuni hii ya Maadili Mema ya Wanafunzi, zinafafanuliwa kama vileo, dawa haramu, dawa za kuagizwa na daktari, kemikali halali zinazoagizwa na daktari au dawa za kununua kwenye kaunti ambazo zinasababisha kudhoofika, na/au kemikali zinazobadilisha mwili au akili au dawa zinazothibitiwa; au dawa zinazowasilishwa kama vileo, dawa haramu, dawa za kuagizwa na daktari, kemikali halali zinazoagizwa na daktari au dawa za kununua kwenye kaunti ambazo zinasababisha kudhoofika, na/au kemikali zinazobadilisha mwili au akili au dawa zinazouzwa kwenye kaunti zinazotumiwa kwa lengo tofauti na lengo lake; au vifaa vya dawa.

Ijapokuwa sio lengo la Bodi au kitivo cha shule na usimamizi kuzuia elimu ya mtu yeyote anayestahiki katika wilaya ya shule, inatambuliwa kwamba nidhamu nzuri shuleni na uraia mwema shuleni ni muhimu kwa mazingira mazuri ya elimu kufanyika. Sio haki kwa wanafunzi wale wanaotaka kunufaika na nafasi zao za elimu na shughuli kuathiriwa na usumbufu usiofaa unaosababishwa na wanafunzi wengine ambao wametumia dawa za kulevya au pombe au wanaomiliki vitu hivi.

Mwanafunzi yeyote anayepatikana kuwa **chini ya ushawishi au anamiliki pombe au dawa za kulevya** anaweza kuondoshwa kwa muda shuleni kwa kipindi cha hadi siku 180 za shule au kufukuzwa shule kabisa. Mwalimu mkuu/mwakilishi **atawaondosha** kwa muda wanafunzi kama hao kwa kipindi cha kwanza cha siku kumi (10) za shule. Kwa makosa ya kwanza ya kumiliki pombe au kumiliki dawa za kulevya, badala ya kuondoshwa kwa muda shuleni kwa siku 10, mwanafunzi huyo anaweza kuchagua kuhudhuria mpango mbadala wa kuingilia kati katika eneo tofauti la shule. Mwanafunzi atahitajika kushiriki katika tathimini kamili ya dawa za kulevya kupitia Kituo Kinachopendelewa cha Afya ya Familia. Mwanafunzi atahudhuria siku nzima ya shule na atakamilisha kazi zote kutoka kwa kozi zake na atapokea mawaidha kuhusu dawa za kulevya/pombe katika siku hizo 10. Wanafunzi wataendelea kupokea msaada kuhusu kutoa maamuzi mema na kuunda uvumilivu baada ya kurudi kwa shuleni yao ya nyumbani. Ikiwa mwanafunzi au mzazi/mlezi hatakamilisha hati zinazohitajika, tathmini au mikutano endelevu ya msaada kwa kuridhisha, kuondoshwa huko kwa kwanza kwa siku 10 kutatekelezwa na Kamati kuhusu Kusikiliza Mienendo itakutana ili kubainisha adhabu inayofaa na/au siku za ziada za kuondoshwa kwa muda shuleni. Pendekezo la adhabu litawasilishwa kwa msimamizi/mwakilishi kwa uamuzi wao.

Baada ya kufanyika tena kwa kosa la pili chini ya Kanuni za Maadili Mema ya Wanafunzi, mwanafunzi huyo ataondoshwa kwa muda shuleni kwa hadi siku 180 za shule au kufukuzwa kabisa.

Kulingana na ukali wa makosa, mwanafunzi aliyepatikana kuwa **ameshiriki katika uuzaji, kushiriki au usambazaji wa pombe au dawa za kulevya** ataondoshwa kwa muda shuleni kwa hadi siku 180 au kufukuzwa kabisa. **Huenda** mwalimu mkuu/mwakilishi akawaondosha kwa muda wanafunzi kama hao kwa kipindi cha kwanza cha siku kumi (10) za shule. Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo unaweza kufanyika ndani ya kipindi cha kuondoshwa kwa muda cha siku kumi (10) za kwanza ili kubainisha adhabu inayofaa. Pendekezo la adhabu linaweza kuwasilishwa kwa msimamizi/mwakilishi kwa uamuzi wao. Afisa wa kusikiliza kesi za Kamati inayohusiana na Mienendo, kwa uamuzi wao, inaweza kupendekeza mahali mbadala pa elimu - Kituo Mbadala cha Masomo (ALC). Ikiwa mpango huo utakubalika: (1) Ndani ya siku mbili (2) za kuanza kwa ALC, lazima tathmini ya dawa za kulevya ikamilishwe katika Kituo Kinachopendelewa cha Afya ya Jamii. (2) Mwanafunzi huyo atahitajika kushiriki katika vikao vya mashauri ya dawa za kulevya vinavyotolewa na Kituo cha Afya ya Familia.

# KANUNI ZA WANAFUNZI ZA MATUMIZI YA POMBE/DAWA ZA KULEVYA

**Ufafanuzi** ufuatayo utatumika:

**“Kuuza, kushiriki na kusambaza”** ina maana ya uhamishaji halisi, uhamishaji wa kubuni, jaribio la kuhamisha au toleo la kuhamisha kutoka mtu mmoja hadi mwingine wa pombe au dawa za kulevya. Neno hili linajumuisha, lakini halijakomea kwa, mauzo, biashara, ubadilishanaji, kushiriki kwenye mitandao ya kijamii na zawadi.

**"Umiliki"** ina maana ya kitendo au hali ya kuwa na pombe au dawa za kulevya kwenye mtu mmoja, ndani au kwenye majengo, yaliyoteuliwa au yaliyokabidhiwa kuwa ya kumdhibiti mwanafunzi.

**"Chini ya ushawishi"** ina maana ya kumeza, kutumia au kufyonza (kwa mdomo, kudunga, kupitia kunusa, n.k) dawa mwilini. “Chini ya ushawishi” inajumuisha, lakini haijakomea kwa, matumizi yoyote ya pombe au dawa za kulevya kabla ya kuwa katika majengo ya wilaya au katika shughuli iliyofadhiliwa na shule au safari ya nje iwe kwenye au mbali na majengo ya wilaya wakati matumizi kama hayo yanaweza kugundulika kwa kuona au kumpima mwanafunzi akiwa shuleni au shughulini. Ikiwa msimamizi anamshuku mwanafunzi kuwa chini ya ushawishi anaweza kutekeleza kipimo cha nje cha utulivu, kuwasiliana na wataalamu wa matibabu au kutekeleza vipimo. Upimaji utajumuisha kipima pumzi cha pombe na kipimo cha mate kwa dawa za kulevya wakati kuna sababu ya kuaminika. Hakuna wakati wowote ufafanuzi wa “chini ya ushawishi” utazuiwa kwa maneno kama yalivyotumika kwa uendeshaji wa magari.

**“Vifaa vya dawa”** ina maana ya vifaa, bidhaa, vitu na nyenzo zote za aina yoyote ambazo zinatumiwa, zinanuiwa kutumiwa, au zimebuniwa kutumiwa katika kuweka, kueneza, kusitawisha, kukuza, kuvuna, kutengeneza, kuchanganya, kugeuza, kuzalisha, kuchakata, kuandaa, kuhifadhi, kuficha, kudunga, kupumua, au kuingiza katika mwili wa mwanadamu dawa iliyothibitiwa au mwigo wa dawa iliyothibitiwa.



# KANUNI ZA SHULE BILA SILAHA

Wilaya ya Shule ya Francis Howell inatafuta kutoa mazingira salama ya elimu yasiokuwa na vurugu kwa wanafunzi wake na maeneo ya kazi ya wafanyakazi wake. Wilaya inathibitisha kwamba silaha hazina mahali popote kwenye maeneo ya shule.

Wilaya inagundua kwamba ni lazima itii sheria za serikali na jimbo kuhusu kuwashughulikia wanafunzi wanaoleta silaha shuleni. Vivyo hivyo, maelezo haya yanatii matoleo ya Sheria ya Kuboresha Shule za Marekani ya 1994, Sheria ya Elimu ya Watu walio na Ulemavu na sheria nyingine husika za serikali na jimbo.

Wilaya inatambua hatari ya madhara ambayo mtu anayeleta bunduki shuleni anaweza kusababisha kwake na kwa wengine katika majengo ya shule. Wilaya inagundua umiliki wa silaha kuwa tishio linalotarajiwa la afya, usalama na usalama wa wanafunzi, wafanyakazi na watu wengine. Wilaya haitavumilia hatari ya madhara yanayoletwa na mtu anayeleta bunduki kwenye majengo ya shule zetu.

Kwa hivyo Wilaya inasema ifuatavyo:

I. UFAFANUZI

Neno "bunduki" limefafanuliwa kulingana na sheria ya serikali kama ilivyowekwa katika toleo jipya la Sheria ya Marekani ya 18 Sehemu ya 921.

Neno "bunduki" linajumuisha, lakini halijakomea kwa, vitu kama vile:

A. Kitu chochote ambacho kimewekwa risasi au silaha isiokuwa na risasi, fremu ya silaha au mtutu wa silaha na ambao umeundwa, au unaweza kubadilishwa kwa urahisi ili kutoa risasi kwa kitendo cha vilipukaji; au
B. Kitu chochote ambacho kinaweza kugeuzwa haraka kutoa risasi kwa kitendo cha vilipukaji au rafadha nyingine, na ambayo ina mtutu ulio na risasi za angalau kipenyo cha nusu inchi; au
C. Kilipukaji chochote, makombora yenye kulipuka, au gesi yenye sumu, kama vile: bomu, grunedi, roketi yenye rafadha ya zaidi ya aunsi nne (4); na vifaa vingine kama hivyo kama vinavyotamubliwa chini ya sheria ya serikali; au
D. Mchanganyiko wowote wa sehemu zilizoteuliwa au zilizokusudiwa kutumiwa katika kugeuza kifaa chochote kama ilivyofafanuliwa katika aya B au C ya sehemu ya Ufafanuzi.

II. WANAFUNZI WANAOLETA BUNDUKI SHULENI

Wilaya haitakubali mwanafunzi kuleta bunduki shuleni. Kwa hivyo, Wilaya itachukua hatua ifuatayo baada ya kubainisha kwamba mwanafunzi ameleta buduki shuleni:

A. Wilaya itamwelekeza mwanafunzi kwa mahakama yanayofaa au mfumo wa mahakama ya watoto; na
B. Wilaya itamwondosha mwanafunzi huyo kwa muda shuleni kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja (1) (siku 365) kuanzia tarehe ya makosa hayo, na huenda, kwa uamuzi wake, ikamfukuza mwanafunzi huyo kabisa shuleni. Toleo hili la kuondoshwa kwa muda linaweza kurekebishwa kulingana na hali baada ya pendekezo la Msimamizi wa Shule ikiwa Msimamizi atabainisha kwamba hali hizo zinafaa mabadiliko hayo.
C. Huenda Wilaya, kwa uamuzi wake, ikampa mwanafunzi aliyeondoshwa kwa muda Chini ya Sera ya Wilaya ya 2620 huduma za elimu katika mazingira mbadala.

III. HALI YA KUTUMIKA KATIKA WANAFUNZI WALIO NA ULEMAVU

Ikiwa mwanafunzi anayebainishwa kuwa anakiuka miongozo hii ya Shule Bila Silaha ni mwanafunzi aliye na ulemavu chini ya Sheria ya Elimu ya Watu Walio na Ulemavu, Wilaya itafuata mahitaji ya serikali na jimbo yaliyowekwa katika sheria na masharti husika. Sheria na masharti kama hayo yaliweka taratibu maalum za kufuatwa wakati mwanafunzi aliye na ulemavu analeta silaha shuleni. Miongozo hii itatumika kwa wanafunzi walio na ulemavu kwa kadri ambayo matumizi yake inaruhusiwa chini ya Sheria ya Elimu ya Watu Walio na Ulemavu.

IV. HALI YA KUTUMIKA KATIKA SERA ZA WILAYA NYINGINE

Sera nyingine zote za Wilaya kuhusu silaha, sera za nidhamu au sera za silaha zinazofanana zitaendelea kutumika kama zilivyo kwa sasa au zilivyotekebishwa hapa.

# UFAFANUZI WA NIDHAMU

**Jumba la Kusoma Kizuizini** - mazingira yanayosimamiwa ya jumba la kusoma lililo nje ya saa za shule. Shule ya Jumamosi ni mazingira yanayosimamiwa ya jumba la kusoma lililo nje ya saa za shule Jumamosi asubuhi. Muda utatofautiana kulingana na shule. Shughuli ya wanafunzi hufuatiliwa kwa karibu na kuzuiwa. Wanafunzi watarajiwa kuwa watulivu wakati wa kipindi chote cha uzuiliwaji na kufanya kazi walizopewa tu. Wanafunzi wanaofika kwa kuchelewa hawataruhusiwa kuingia.

**Kuondoshwa kwa Muda Darasani (ISS/ISAP)** - mazingira yaliyopangwa, ya kibinafsi ambapo mwanafunzi atapewa nafasi ya kukamilisha kazi ili kupata sifa. Mzazi/mlezi atapigiwa simu kabla ya mwanafunzi kuwekwa katika ISS/ISAP. Ikiwa mwanafunzi aliye na IEP atawekwa katika ISS/ISAP, huduma yake ya elimu maalum itatolewa kama ilivyoelezewa katika IEP au muda katika ISS/ISAP utachukuliwa kama kuondoshwa kwa muda shuleni. Mwanafunzi anaweza kushiriki katika shughuli baada ya kukamilisha kuondoshwa kwake kwa muda darasani.

**Kuondoshwa kwa Muda Shuleni (OSS)** - kuondolewa ili usihudhurie shule. Mkutano wa mwanafunzi na mzazi/mlezi unaweza kuhitajika kabla ya mwanafunzi kurudi shuleni. Wanafunzi wanaopokea OSS watakuwa na nafasi ya kurudia kazi zao walizokosa kwa sifa za asilimia 100 isipokuwa kwa hali zilizoashiriwa hapa chini.

Gredi ya mwanafunzi wakati wa muda wa kuondoshwa kwa muda itategemea kazi ambayo ilitolewa kwa mwanafunzi kukamilisha nje ya darasa wakati wa kipindi cha kuondoshwa kwa muda. Ikiwa mwanafunzi atapewa mazingira mbadala na mazingira haya yakataliwe, mzazi/mlezi atawajibika kwa elimu ya mwanafunzi huyo kwa muda uliosalia wa kuondoshwa kwa muda.

HAKUNA KAZI YA MARUDIO ITAKAYORUHUSIWA IKIWA:

- Kazi inayopaswa kurejeshwa ya OSS haijawasilishwa kabla ya tarehe inayofaa
- Kazi inayopaswa kurejeshwa ya ISS/ISAP haijakamilishwa kabla ya siku ya mwanafunzi huyo kurudi darasani
- Mwanafunzi/Mzazi/Mlezi anachagua kutofanya AIP (Mpango Mbadala wa Kuingilia Kati)
- Kuondoshwa kwa muda ni kwa zaidi ya siku 55 za shule

Mwanafunzi yeyote anayeondoshwa kwa muda shuleni huenda asiwe kwenye majengo ya shule au majengo mengine yoyote ya Wilaya wakati wa muda wa kuondoshwa kwa muda shuleni. Isitoshe, huenda mwanafunzi aliyeondoshwa kwa muda asishirki wala kuhudhuria shughuli yoyote ya masomo aidha ndani au nje ya kampasi wakati wa muda wa kuondoshwa kwake.  Baada ya kukamilisha kuondoshwa kwake kwa muda shuleni, lazima mwanafunzi aweze kuaminika tena kama raia mwema wa shule kabla ya kushiriki au kushindana katika shughuli. Hata hivyo, mwanafunzi anaruhusiwa kwenye majengo ya Wilaya ili kuhudhuria Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo na kuhudhuria mpango mbadala aliopewa.

Mwanafunzi yeyote anayerudi shuleni kufuatia kuondoshwa kwa muda shuleni lazima ahudhurie mkutano wa kurudi tena unaohusisha mwalimu mkuu/mwakilishi na unaweza kujumuisha mzazi/mlezi wa mwanafunzi.

**Kuondoshwa kwa muda shuleni kwa siku 10 hadi 180** –Msimamizi /mwakilishi anaweza kumwondosha kwa muda mwanafunzi kwa hadi siku 180 za shule na kupendekeza muda zaidi wa kuondoshwa na hata kufukuzwa kabisa na Bodi ya Elimu. Ni Bodi pekee inaweza kuidhinisha kuondoshwa kwa muda wa zaidi ya siku mia moja na themanini (180). Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo utafanyika ili kupitia matokeo ya tabia baada ya kuondoshwa kwa muda kwa mara ya kwanza na kutoa pendekezo kuhusu kuondoshwa kwa muda kwa zaidi ya siku kumi (10) za shule na/au kufukuzwa kabisa.

# UFAFANUZI WA NIDHAMU

**Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo** - Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo utafanyika kabla ya utekelezaji wa kuondoshwa kwa muda nje ya shule wa zaidi ya siku kumi (10) za shule. Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo utakuwa na afisa wa kusikiliza, mwalimu mkuu/mwakilishi na wafanyakazi wengine wa jengo au wilaya ikiwa itakuwa muhimu. Mwanafunzi na wazazi/walezi wake watapewa nafasi ya kutokea mbele ya Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo. Usikilizaji huo utafanyika wakati wa kipindi cha kwanza cha siku kumi (10) za shule cha mwanafunzi kuondoshwa kwa muda. Mawakili hawaruhusiwi kuhudhuria Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo (kando na mzazi/mlezi ambaye ni wakili na anahudhuria na mtoto wake mwenyewe). Vifaa vya kurekodi haviruhusiwi katika Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo isipokuwa ni muhimu ili kukimu ulemavu wa mzazi/mlezi. Taarifa ya hitaji la kutumia kifaa cha kurekodi kama msaada lazima ipokewe na Idara ya Huduma za Wanafunzi angalau saa 48 kabla ya usikilizaji.

Mwanafunzi anayeondoshwa kwa muda shuleni kwa zaidi ya siku kumi (10) na mwakilishi wa msimamizi anaweza, ndani ya siku kumi (10) za kupokea ilani ya kuondoshwa huko kwa muda, anaweza kuomba rufaa ya uamuzi wa Kamati ya Mienendo kwa Msimamizi wa Shule ikiwa ana maelezo anayoamini hayakuzingatiwa wakati wa usikilizaji. Lazima maombi kama hayo yapokewe katika ofisi ya Msimamizi kabla ya saa 4:30 p.m. ya tarehe ambayo ombi hilo linafaa. Mawakili hawaruhisiwi kuhudhuria mkutano wa rufaa na Msimamizi wa Shule.

Ikiwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi hatakubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Shule, ombi linaweza kuombwa la usikilizaji mbele ya Bodi ya Elimu. Mwanafunzi anayeomba usikilizaji huo ataarifiwa kwa kuandikiwa kuhusu mashtaka dhidi ya mwanafunzi huyo; saa, tarehe, na eneo la usikilizaji; na haki ya mwanafunzi ya kuwakilishwa na wakili, kuwaita mashahidi na kuwauliza maswali, na kutoa ushahidi wowote unaomtemtea mwanafunzi.

**Toleo la Nidhamu ya Elimu Maalum *(Wanafunzi walio na Ulemavu)*** - Wanafunzi wanaopokea kwa sasa huduma za elimu maalum wataadhibiwa kulingana na amri ya jimbo na serikali. Katika visa ambavyo wanafunzi walio na ulemavu wanapendekezwa kwa Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo, na matokeo ya usikilizaji huo yanahusisha kuondoshwa kwa muda wa siku 10 za shule, mkutano wa Kubainisha Udhihirisho utafanyika ili kubainisha kama makosa yalihusiana na ulemavu wa mwanafunzi au la kufuatia usikilizaji wa Kamati ya Mienendo.

**Sera ya Raia wa A+ ya Wanafunzi wa Shule ya Upili**
Kamati ya Ushauri wa A+ ya Wilaya ya Shule ya Francis Howell inaamini kwamba uraia mwema ni muhimu kwa wanafunzi wanaohitimu na sifa ya A+. Wanafunzi wanaoshiriki katika mpango wa A+ wanaoondoshwa kwa muda wanahatarika kustahiki kwao. Miaka yote minne ni sehemu ya rekodi ya uraia. Matokeo yafuatayo yatasababisha kuondolewa kwa Mpango wa A+:

- Matukio 5 au zaidi ya kuondoshwa kwa muda darasani/shuleni wakati wa siku ya wanafunzi ya maonyesho ya kazi ya shule ya upili (gredi ya 9-12).
- Kuondoshwa kokote ambao kunasababisha kuondoshwa kwa muda darasani au shuleni kwa zaidi ya siku 10 au zaidi.

**Mchakato wa Rufaa ya A+**
Mwanafunzi na/au mzazi/mlezi ana haki ya kuomba rufaa ya A+ baada ya kupokea ilani ya makosa ya kuhudhuria au ya uraia.
Katika visa vya wasiwasi au kutostahiki:

- Lazima mwanafunzi na mzazi/mlezi aarifu Mratibu wa A+ kwa kumwandikia kuhusu lengo lake la kujadili wasiwasi huo au kustahiki.
- Mratibu wa A+ ataita mkutano wa Kamati ya Rufaa ya A+ ili kuzingatia ustahiki.
- Kamati ya Rufaa ya A+ itasikia ombi na kurudisha uamuzi wake kwa mwanafunzi na mzazi/mlezi.

Mtu yeyote anayeomba rufaa anapaswa kukamilisha fomu ya “Rufaa ya A+” ambayo inapatikana kutoka kwa mratibu wa A+ katika shule ya upili ya mwanafunzi. Baada ya kamati ya kupitia kufikia uamuzi wake, Mratibu wa A+ atawaarifu wazazi/mlezi.

# UFAFANUZI WA NIDHAMU

**Kufukuzwa kabisa –** Neno kufukuzwa kabisa linarejelea kufukuzwa kabisa shuleni. Kwa kuongezea kuweka vikwazo vya kuondoshwa kwa muda mrefu, Msimamizi wa Shule anaweza kupendekeza kwa Bodi ya Shule kwamba mwanafunzi afukuzwe kabisa shuleni. Bodi itapitia mapendekezo hayo na kuamua kama itaendelea na usikilizaji wa kufukuzwa kabisa. Ikiwa Bodi ya Elimu itaendelea na usikilizaji wa kufukuzwa kabisa, mwanafunzi na wazazi/walezi wataarifiwa kwa kuandikiwa kuhusu mashtaka dhidi ya mwanafunzi; saa, tarehe na eneo la usikilizaji; na mwanafunzi ana haki ya kuwakilishwa na wakili, kuwaita mashahidi na kuwauliza maswali, na kuwasilisha ushahidi wowote unaomtetea mwanafunzi. Hakuna mwanafunzi atakayefukuzwa kabisa bila kusikilizwa mbele ya Bodi ya Elimu.

Kulingana na Sera ya Wilaya ya 2660, hakuna mwanafunzi atarudishwa shuleni au kuruhusiwa kuandikishwa (isipokuwa inahitajika kisheria) kufuatia kuondoshwa kwa muda au kufukuzwa kabisa kutoka Wilaya hii au kutoka Wilaya nyingine yoyote ya Shule hadi wilaya ifanye mkutano wa kuzingatia uwezo wake wa kuchukuliwa tena. Wakati wa mkutano huu, washiriki watazingatia mienendo ambayo ilisababisha hatua za kinidhamu na hatua zozote za marekebisho zinazoaminika kuwa muhimu ili kuzuia matukio ya baadaye ya tabia kama hiyo.

Hata hivyo, hakuna mwanafunzi atakayechukuliwa tena au kuandikishwa tena ikiwa mwanafunzi huyo ameshtakiwa, kuhukumiwa kama mtu mzima au mtoto bila uamuzi wa mwisho, au kushtakiwa kwa makosa ya watoto, ambayo kama atashtakiwa kama mtu mzima, itakuwa ni mojawapo ya makosa yafuatayo:

- Mauaji yaliyopangwa mapema (Mo. Rev. Stat. § 536.020)
- Mauaji ya makusudi ambayo hayakupangwa mapema (Mo. Rev. Stat. § 565.021)
- Mashambulizi ya kusababisha madhara makubwa ya kimwili (Mo. Rev. Stat. § 565.050)
- Ubakaji (Mo. Rev. Stat. § 566.030)
- Ulawiti (Mo. Rev. Stat. § 566.060)
- Wizi wa kimabavu (Mo. Rev. Stat. § 570.023)
- Usambazaji wa dawa za kulevya kwa watoto (Mo. Rev. Stat. § 579.020)
- Uchomaji kwa lengo la kuharibu mali (Mo. Rev. Stat. § 569.040)
- Utekaji Nyara kama kosa la Daraja A (Mo. Rev. Stat. § 565.110)
- Ubakaji wa watoto (Mo. Rev. Stat. § 566.032)
- Ulawiti wa watoto (Mo. Rev. Stat. § 566.062)

# MIONGOZO YA BASI




Madereva wa mabasi ya Francis Howell wamevikwa majukumu ya kudumisha mazingira salama na mema katika mabasi ya wilaya.

Ifuatayo ni orodha ya matarajio ya wanafunzi wakiwa ndani ya mabasi ya wilaya:

- Fuata matarajio yote katika Kanuni za Maadili Mema ya Wanafunzi
- Fuata maagizo yote ya dereva wa basi
- Endelea kuketi ukiwa umeangalia mbele ya basi
- Dumisha matarajio ya kutotangamana na watu
- Panga na ushuke basi katika vituo vilivyoteuliwa
- Weka sehemu zote za mwili na vitu vyote ndani ya basi
- Watendee wengine kwa heshima (kwa maneno na kimwili)
- Shughulikia basi kwa heshima (hakuna uharibifu wa vitu, kutupa taka, kurusha vitu, kula au kunywa)
- Panda basi ulilotеuliwa

KUMBUKA: Huenda mabasi yote yakafuatiliwa na kamera wakati wowote ule.

**Ili kudumisha mpangilio na kutoa mazingira salama, dereva wa basi anaweza kuchukua yoyote kati ya hatua zifuatazo:**

- Kuanzisha mkutano na mwanafunzi
- Kuanzisha mkutano na mwalimu mkuu/mwakilishi
- Kuwaelekeza wanafunzi kutii sheria
- Kupangia viti vya basi
- Kupeana maonyo ya tikiti za basi
- Kupeana tikiti za basi

**Wilaya itachukulia basi kuwa mwendelezo wa darasa; kwa hivyo, mwenendo wowote mbaya kwenye basi utakuwa na matokeo. Matokeo yanaweza kujumuisha kuondoshwa kwenye basi.** Katika visa ambavyo ukiukaji ni mkali na/au unatishia usalama wa jumla wa wanafunzi suala hilo litaelekezwa mara moja kwa mwalimu mkuu/mwakilishi. Mwalimu mkuu/mwakilishi kwa uamuzi wake anaweza kutekeleza/kuanzisha mpango mbadala wa nidhamu ukihitajika. Mkurugenzi wa Wilaya wa Usafiri na Meneja wa Usalama wa Usafiri watakutana na mwalimu mkuu/mwakilishi kama ilivyoombwa au wakati inahitajika.

# ADHABU ZA VIBOKO: ZIMEPIGWA MARUFUKU

Sera ya Wilaya 2670 inasema: Hakuna mtu aliyeajiriwa au kujitolea wa Wilaya atamwadhibu au kusababisha kuadhibiwa kwa viboko mwanafunzi anayehudhuria shule za Wilaya.

Mfanyakazi wa wilaya anaweza kutumia udhibiti unaoeleweka dhidi ya mwanafunzi bila ilani ya mapema ya mwalimu mkuu/mwakilishi ikiwa ni muhimu kujilinda mwenyewe, kudumisha mpangilio, au kuwakinga watu wengine a mali ya Wilaya.



# MTANDAO na MIONGOZO INAYOKUBALIKA YA MATUMIZI YA INTANETI

Ufikiaji wa Intaneti unapatikana katika Wilaya ya Shule ya Francis Howell (FHSD) kwa wanafunzi, walimu, wafanyakazi, wazazi/walezi na wasimamizi. Lazima wanafunzi watumie mawasiliano ya FHSD kulingana na Sera ya Wilaya ya 6320. Wanafunzi wanaruhusiwa kufikia maelezo yanayohusiana na mtaala na kutafuta mada na dhana ambazo zinakuza uvumbuzi katika elimu.

Kujifunza jinsi ya kuwasiliana kwa njia pepe na kupitia maelezo mengi yaliyo kwenye mitandao ya umma na ya kibinafsi ni ujuzi wa kusoma na kuandika ambao unaunga mkono mafanikio ya mwanafunzi katika karne ya 21. Katika hali nyingine, wanafunzi, wakiidhinishwa na mwalimu wa darasa, wataruhusiwa kuleta teknolojia zao wenyewe kwa madhumuni ya elimu (k.m. vipakatalishi, iPods, iPads, visomaji vya kielektroniki, n.k.).

**Usalama**
Wilaya uhakikisha utiifu wa CIPA (Sheria ya Ulinzi wa Intaneti ya Watoto) kupitia matumizi ya ng'ome na uchujaji. Hata hivyo, wanafunzi wanapaswa kuripoti kwa mwalimu wao au wafanyakazi wengine ikiwa watafikia maelezo ambayo yanawafanya wasijihisi vizuri.

Hatua zifuatazo zinaruhusiwa kwenye mitandao ya wilaya:

- Matumizi ya mawasiliano kwa malengo ya elimu pekee
- Kuwasiliana na wengine kwa njia ya heshima na ukarimu
- Kutii sheria za hakimiliki na haki za rasilimali ya akili za wengine
- Kudumisha usiri wa majina ya kibinafsi, nambari za simu, anwani na manenosiri, na kuheshimu usiri huo wa watu wengine

Miongozo hii imetolewa ili ufahamu kuhusu majukumu yako. Msimamizi wa mtandao au mwakilishi aliyeteuliwa wa FHSD anaweza kubadilisha haki za mtandao/kompyuta ikiwa miongozo hii haitazingatiwa.

Hatua zifuatazo **HAZITARUHUSIWA** kwenye mitandao ya wilaya:

| | |
|---|---|
| Kushiriki maelezo ya siri | Kupeana manenosiri kwa wengine |
| Kupeana maelezo ya kibinafsi kwenye Intaneti | Kunyanyasa, kutukana, au kuwadhuru wengine kwa njia yoyote ile |
| Kufikia nyenzo za ponografia/za kinyume cha sheria | Kujaribu kuruka au kubatilisha mfumo wa usalama |
| Kunakili programu kinyume cha sheria | kuingia kwenye folda, faili au hati za wengine bila |
| ruhusa Kujaribu kuharibu data/faili za wengine | Kutumia mtandao kwa malengo ya kibiashara |
| Kutumia lugha chafu | Kutumia michezo ya Intaneti isio ya mtaala |
| Kukiuka sheria za hakimiliki au wizi wa maandishi | Kutumia tovuti zisizoidhinishwa |
| Kuharibu mtandao au teknolojia ya Wilaya | Kupakia virusi, kubadilisha data au wizi wa maelezo yaliyozuiwa |

**HATUA ZINAZOWEZEKANA ZA KINIDHAMU KWA AJILI YA UKIUKAJI**
Ukiukaji wa Sera ya Wilaya ya 6320 kuhusu matumizi ya mtandao na intaneti utasababisha hatua za kinidhamu kuchukuliwa ambazo zinajumuisha, lakini hazijakomea kwa, moja au zaidi ya zifuatazo: 1) kusitishwa au kubatilishwa kwa haki za mtandao; 2) kuondoshwa au kubatilishwa kwa ufikiaji wa Intaneti; 3) kuondoshwa au kubatilishwa kwa ufikiaji wa kompyuta; 4) kuondoshwa kwa muda shuleni; au 5) kufukuzwa kabisa.
**<u>TAFADHALI KUMBUKA:</u> Ikiwa ungetaka kukataza matumizi huru ya intaneti kwa mwanafunzi wako, tafadhali wasiliana na shule anayehudhuria ili upate fomu inayofaa.**

# KAMUSI YA MANENO

**Udhalimu**
Udhalimu umefafanuliwa katika Sera ya 2655 ya Bodi ya Elimu kama hatua ya makusudi ya mtu au makundi ya watu ya kutoa vitisho, tabia ya fujo, au ya unyanyasaji ambayo inajirudia au inaweza kurudiwa na inayomfanya mwanafunzi kuwa na hofu ya usalama wake wa kimwili au wa mali; ambayo hutatiza utendakazi wa elimu, nafasi, au haki za mwanafunzi yeyote; au hutatiza shughuli za kawaida za shule. Udhalimu unaweza kujumuisha vitendo vya kimwili, vikiwemo ishara, au udhalimu wa maneno, kielektroniki, au mawasiliano ya kuandikwa, na tishio lolote la kulipiza kisasi kwa kuripoti vitendo vya udhalimu.

Wilaya imejitolea kudumisha mazingira ya kusoma na kufanya kazi yasiokuwa na aina yoyote ya udhalimu au vitisho kutoka kwa wanafunzi katika maeneo ya shule, wakati wa shule, katika shughuli zilizofadhiliwa na shule au katika muktadha unaohusiana na shule. Wanafunzi na/au wazazi/walezi wao wanahimizwa kuripoti matukio yoyote ya udhalimu kwa msimamizi wa jengo.

Wilaya inawahimiza wanafunzi kuripoti udhalimu. Wanafunzi wanapaswa kuripoti ikiwa hao ni waathiriwa au ni watazamaji. Shule zitajadili njia salama za kuripoti udhalimu na wanafunzi. Wanafunzi wanaoonewa au kushuhudia maonevu wanapaswa kuripoti tukio hilo moja kwa moja kwa mtu mzima. Wazazi / walezi wanapaswa kuwasiliana na mwalimu mkuu ili kuripoti udhalimu ulioripotiwa na mtoto wao ikiwa mtoto hako sawa kutoa ripoti. Kila ripoti ya udhalimu itachunguzwa. Tovuti ya FHSD ina rasilimali za udhalimu kwa wazazi na wanafunzi chini ya kichupo cha Wazazi kwenye tovuti ya Wilaya. http://fhsd.sharpschool.net/parents/bullying/

**Mkutano**
Mawasiliano ambayo hufanyika ana kwa ana, kwa video au kwa simu.

**Udhalimu wa mtandaoni**
Udhalimu wa mtandaoni kama ulivyofafanuliwa katika Sera ya 2655 ya udhalimu kama ilivyofafanuliwa hapo juu kupitia upitishaji wa mawasiliano ikiwemo, lakini haijakomea kwa, ujumbe, matini, sauti au picha kwa njia za vifaa vya elektroniki vikiwemo, lakini havijakomea kwa, simu, simu pasiwaya au kifaa kingine chochote cha mawasiliano pasiwaya, kompyuta, au peja. Huenda wilaya ikapiga marufuku au kuchukua hatua za kinidhamu kwa udhalimu wa mtandaoni ambao unatoka katika kampasi yoyote ya Wilaya au katika shughuli ya Wilaya ikiwa mawasiliano ya elektroniki yalifanywa kwa kutumia rasilimali za kiteknolojia za shule, ikiwa kuna uhusiano wa kutosha na mazingira ya elimu, au ikiwa mawasiliano ya elektroniki yalifanywa kwenye kampasi ya Wilaya au shughuli ya Wilaya kwa kutumia rasilimali za mwanafunzi za kiteknolojia. Isitoshe, wanafunzi wanaoshiriki katika vitendo vikubwa vya mienendo mibaya nje ya kampasi ambayo mwishowe huathiri pakubwa elimu ya wanafunzi wa Wilaya watachukuliwa hatua za kinidhamu.

**Unyanyasaji/Ubaguzi**
Ni sera ya Wilaya kudumisha mazingira ya elimu ambayo hayana unyanyasaji kwa sababu za umbari, rangi, jinsia, asili ya kitaifa, jamii, ulemavu, dini, mapendeleo ya kingono au mwelekeo wa kingono unaoshukiwa. Wilaya imepiga marufuku aina zote za unyanyasaji na ubaguzi kwa sababu za umbari, rangi, jinsia, asili ya kitaifa, jamii, ulemavu, dini, mapendeleo ya kingono au mwelekeo wa kingono unaoshukiwa.

Mfumo wa shule utachukua hatua mara moja ili kuchunguza malalamiko yote, yawe rasmi au yasio rasmi, ya kutamkwa au ya kuandikwa, ya unyanyasaji au ubaguzi kwa sababu za umbari, rangi, jinsia, asili ya kitaifa, jamii, ulemavu, dini, mapendeleo ya kingono au mwelekeo wa kingono unaoshukiwa; mfumo huu utachukua hatua zinazofaa ili kuwalinda watu dhidi ya unyanyasaji au ubaguzi zaidi; na, ikiwa itabainishwa kwamba unyanyasaji au ubaguzi ulifanyika, kuchukua hatua za haraka na zinazofaa za kinidhamu dhidi ya mwanafunzi, mwalimu, msimamizi au mfanyakazi yeyote yule atakayepatikana kuwa alinyanyasa/kubagua, na/au kuchukua hatua nyingine mwafaka zinazofaa ili kukomesha unyanyasaji.

# KAMUSI YA MANENO

**Udhalilishaji**

Udhalilishaji wa wanafunzi umepigwa marufuku kabisa na Sera ya Wilaya ya 2920. Udhalilishaji umefafanulia kama tabia ya makusudi inayoelekezewa mwanafunzi mwingine, iwe inafanyika katika majengo ya shule au nje, kwa malengo ya kumwingiza au kumsajili kwa shughuli yoyote inayohusiana na shule au timu ya riadha. Tabia zinazopigwa marufuku na sera hii zinajumuisha, lakini hazijakomea kwa, kuonekana au kuguswa kwa sehemu nyeti, makalio, au matiti (wanafunzi wa kike) moja kwa moja au kwa njia isio ya moja kwa moja kupitia kugusana na nguo za ndani; vitisho vya madhara ya kimwili; na kusababisha madhara ya kimwili au ya kiakili au aibu.

Wanafunzi watakaopatikana wakikiuka sera hii wataondoshwa kwa muda/kufukuzwa shuleni kabisa na kuondoshwa kwa muda na kufukuzwa kabisa katika shughuli/kushiriki katika riadha kulingana na ubaya wa tabia hiyo.

**Vibali vya Kuegesha Gari**

Kwa sababu ya nafasi isiotosha inayopatikana ya wanafunzi kuegesha magari katika kila kampasi ya shule ya upili, vibali vya kuegesha magari vinahitajika kwa wanafunzi kuendesha shuleni. Kigezo cha kustahiki vibali na sheria nyingine zinazohusiana na magari ya wanafunzi zitawekwa na msimamizi anayefaa wa shule ya upili. Huenda ukiukaji ukasababisha kupoteza haki za kuegesha gari.

**Urejeshaji**

Kurudisha bidhaa ambazo ziliibwa au kuharibiwa au kutoa thamani nzuri ya soko kwa njia ya fidia au huduma.

**Kuiba/Wizi**

Kuchukua au kujaribu kuchukua mali ya mtu au taasisi nyingine bila ruhusa au ufahamu wa mmiliki na lengo la kumnyima mmiliki matumizi yake (chini ya kosa la Wizi)

**Sexting**

Utumaji wa picha au ujumbe waziwazi wa kingono kupitia kifaa cha elektroniki.

**Tisho la Kigaidi** **s**

Ikiwa mtu yeyote atatishia au atatekeleza ukatili kwa lengo la kumtishia mtu mwingine au kusababisha wasiwasi kwa umma.

**Kupita bila ruhusa**

Kuwa katika majengo ya shule bila ruhusa, ikiwemo wakati umeondoshwa kwa muda au kufukuzwa kabisa; pamoja na kuvunja na kuingia kwa nguvu. Au kubaki shuleni baada ya usimamizi wa shule kuomba mtu husika aondoke shuleni.

**Silaha (ikiwemo vitu vinavyofanana na silaha na risasi)**

Silaha ni, kwa njia ya maonyesho na bila kikomo, mojawapo ya zifuatazo:

- Bunduki: Bunduki kama ilivyofafanuliwa katika 18 U.S.C. 921 ya sheria za serikali. Mifano ya bunduki ni bastola, bunduki ya marisau na bomu. Rejelea sheria ya serikali kwa ufafanuzi kamili.
- Bunduki Zingine: Bunduki ya aina yoyote, iwe ina risasi au haina risasi, inayofanya kazi au isiofanya kazi, pamoja na kitu chochote kando na bunduki ambacho kinafanana na bunduki. Hii itajumuisha, lakini haitakomea kwa, bunduki ya marisawa, bunduki ya rangi, bunduki ya kushtua, bunduki ya umeme, bunduki ya BB, bunduki ya fataki, bunduki ya misumari na bunduni ya michezo.
- Silaha Nyingine: Kitu au kifaa chochote kinachotumiwa kwa njia ya kutishia ambacho kinaweza kusababisha au kimekusudiwa kusababisha madhara ya kimwili na/au majeraha, kando na bunduki. Hii itajumuisha, lakini haijakomea kwa, kisu kinachoweza kubadilishwa, kisu cha kuwinda, kisu kama nyota, wembe (pamoja na wembe mnyoofu au wa kujirudisha ndani) vyuma vya ngumi, kikata sanduku, silaha yenye vijiti viwili, glovu zenye ncha, bambo la mkononi lenye ncha, rungu yoyote, kifaa cha kutoa machozi au bidhaa ya maji ya kuwasha.

Sheria ya Jimbo la Missouri inayofafanua silaha inaweza kupatika katika kiungo kifuatacho:
http://www.moga.mo.gov/statutes/C500- 599/5710000010.HTM